

Mfumo e-Mrejesho wang'ara tuzo za Umoja wa Mataifa

Dar es Salaam

NA MWANDISHI WETU

TANZANIA imeshinda tuzo za Umoja wa Mataifa ya ubunifu katika huduma za umma kwa mwaka huu kupitia mfumo wa e-Mrejesho.

Mfumo huo umetambuliwa na Umoja huo kama jukwaa linaloweza serikali kukusanya maoni na malalamiko ya wananchi kwa njia ya kidijitali, hivyo kufanya uamuzi wa sera na utekelezaji kwa wakati.

Hafla ya utoaji wa tuzo za Umoja wa Mataifa kuhusu Huduma za Umma ilifanyika Juni 26, mwaka huu katika kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ya Umoja wa Mataifa jiji la Incheon, Jamhuri ya Korea.

Tanzania ilikuwa kati ya nchi mbili tu za Afrika zilizotunukiwa tuzo hiyo, nyingine ikiwa ni Afrika Kusini ambapo jumla ya nchi 73 wanachama wa Umoja wa Mataifa zilishiriki na mifumo 400 iliwasilishwa wakati mifumo 15 pekee ndiyo ilishinda tuzo mbalimbali ukiwemo mfumo wa e-Mrejesho.

Tuzo hizo zilitolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika Idara ya Masuala ya Kiuchumi na ya Kijamii, Li Junhua na Waziri wa Mambo ya Ndani wa Korea, Lee Sang-min na kupokelewa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Xavier Daudi.

Mfumo wa e-Mrejesho uliosanifiwa na kutengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, unaruhusu wananchi kuwasiliana na taasisi zote za Serikali na kuwasilisha maoni, malalamiko au pongezi.

Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Mhandisi Benedict Ndomba alieleza kuwa, tuzo hiyo inaonesha utambuzi wa mchango mkubwa wa mfumo wa e-Mrejesho duniani kama jukwaa huru linalowaunganisha wananchi na serikali katika kuboresha utawala wa demokrasia kupitia teknolojia.

Aliongeza, mfumo huu unaruhusu serikali kukusanya malalamiko, maswali na maoni ya wananchi na kuyafanyia kazi kwa wakati na unamwezesha mwananchi kutuma maoni yake bila kujulikana endapo hataki kujulikana.

"Mfumo wa e-Mrejesho ni jukwaa huru kwa kuwa umezingatia faragha za wananchi, ambapo kwa wale wasiopenda kujulikana wanapowasilisha maoni yao serikalini wanaweza kuwasilisha bila kujulikana, hivyo kuhakikisha sauti za watu zote zinasikilizwa, hii inachochea utamaduni wa uwazi na uwajibikaji katika taasisi za umma," alisema.

Mhandisi Ndomba alisema mfumo wa e-Mrejesho ni hatua kubwa katika juhudi za e-GA za kujenga daraja kati ya serikali na wananchi wake na kuwa, ushindi wa tuzo hiyo kutoka Umoja wa Mataifa unaonesha namna azma ya e-GA ya kukuza uwazi na uwajibikaji katika utawala wa umma kupitia teknolojia inavyotekelezwa.

Aidha, alibainisha kuwa, ikiwa mwananchi atakosea kuwasilisha lalamiko lake katika taasisi husika, mfumo wa e-Mrejesho unaruhusu lalamiko hilo kuhamishwa kutoka taasisi moja kwenda taasisi nyingine na unamruhusu mwananchi kukata rufani kwenda ngazi ya juu ya taasisi ikiwa hatoridhika na majibu yaliyotolewa kuhusu lalamiko lake.

"Mfumo huu unasaidia kuongeza uwajibikaji, kwani lalamiko linapofika katika taasisi litaonekana ngazi zote za uongozi wa taasisi hiyo na kila ofisa aliyelifungua ama kulifanyia kazi ataonekana, pia mfumo unafanya uchambuzi wa taarifa na kumwezesha Katibu Mkuu Ofisi ya Rais UTUMISHI na Katibu Mkuu Kiongozi kuona malalamiko yaliyowazi, yanayoshugulikiwa na yaliyokamilika kupitia 'dashboard' maalumu," alisema.

Machi 13, mwaka huu, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, aliwataka viongozi wa umma kutumia Mfumo e-Mrejesho kupokea maoni ya wananchi kuhusu serikali na kutoa mrejesho kwao kupitia mfumo huo kuimarisha uwajibikaji kwa viongozi wa umma.